

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA  
OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKOND VIHOKOLI

S.L.P 221

NEWALA

TAREHE.....

MWANAFUNZI.....

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI VIHOKOLI MWAKA 2021.**

Ninafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021, shule ipo kilometra 53 kaskazini mwa makao makuu ya wilaya ya newala , shule ni ya kutwa na ni mchanganyiko .

**shule itafunguliwa tarehe 11-01-2021 saa 07:00 asubuhi.**

**1.0: MAHITAJI MUHIMU YA SHULE**

**2.0: SARE ZA SHULE**

**[A] WAVULANA**

(1)shati nyeupe 2 mikono mifupi , zisibane na zisiwe pana sana/.

(2) suruali 2 za rangi ya bluu bahari zisiwe pana sana na zisibane ziwe za malinda mbele. mifuko isiwe ya mshono wa jeans.

(3) viatu vyeusi vyta ngozi jozo 2

(4)soksi nyeupe jozo 2

(5) raba rangi ye yeyote kwa ajili ya michezo

(6)fulana 2 nyekundu kwa ajili ya michezo

(7) track suit 2 nyekundu 2 kwa ajoili ya michezo

(8)mchango kwa ajoili ya mwalimu anaajitolea kufundisha (biology+physics) **sawa na tsh/=10000.**

## **(B) WASICHANA**

- (1) shati nyeupe 2 mikono mifupi , zisibane na zisiwe pana sana
- (2) sket 2ndefu zinazovuka magoti rangi ya bluu bahari.
- (3) viatu vya ngizi jozi 2
- (4) soksi nyeupe kwa ajili ya michezo .
- (5) raba rangi ye yote kwa ajili ya michezo
- (6) sketi nyeupe kwa ajili ya kazi za nje , fulana nyekundu kwa ajili ya michezo
- (7) hijabu inaruhusiwa ila iwe ya nusu kanzu , suruali na juba visibane , visiwe pana sana kama ni sketi iwe ndefu ya kuvuka magoti.
- (8) mchango kwa ajili ya mwalimu wa kujitolea **10000/= kwa mwaka 2021**

## **2.2: VIFAA VYA USAFI**

- i. Ndoo moja ndogo
- ii. Jembe moja lenye mpini
- iii. Fagio moja imara

## **2.3:VIFAA VYA DARASANI**

- () kalamu
- ()mkebe (mathematical set)
- ()daftari kubwa 12
- ()rula moja
- ()rim paper moja au pesa taslimu (12000/=)
- () kamusi moja (dictionary) au pesa taslimu (12000/=)

## **3.0 MAMBO MUHIMI YA KUKAMILISHA**

KABLA HUJAFIKA SHULENI KAMILISHA MAMBO YAFUATAYO

(A) medical examination fotrm ambayo itajazwa na mganga ,mkuu wa hospitali ya serikali. fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara tu utakapo ripoti shulen .

(B) fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi / mkataba wa kutoshiriki katika mgomo , fujo na makosa ya jinai.

(C) Fomu ya uraia au ulete nakala ya cheti cha kuzaliwa .

(D) fomu ya kukili kanuni na sheria za shule.

4.0: T afadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamiloifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI VIHOKOLI

.....  
LUFINGO T. MWAIJANDE

MKUU WA SHULE

MAWASILIANO: 0689851755/0672610517

**MAAGIZO MUHIMU**

1. ukiwa nyumbani utatakiwa kuzisoma kwa makini sheria za shiule ambazo zitakuwA mwongozo wako siku zote za maisha yako hapa shulen. baada ya kusoma na kuzielewa utatakiwa kujaza fomiu namba mbili kAMA kiapo cha kuzielewa na kukubali kuishi kwa mujibu wa sheria za shule. fomu hii utatakiwa kuikabidhi kwa mwalimu atakaekupokea.
2. Makosa yanayoweza kusABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI:
  - ( ) WIZI
  - ( ) uasherati,ushoga kulawit na kubaka
  - 3. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevyta
  - 4. Uvutaji wa bangi
  - 5. Makosa ya jinai
  - 6. Kupigana kupiga au kusababisha ugomvi
  - 7. kuharibu kwa makusudi mali ya uma au kuiipoteza
  - 8. Kudharau bendera ya taifa
  - 9. Kugoma, kuchochea na kuongoza vurugu hivyo kuvunja amani na usalama shulen au jamii inayokuzunguka.
  - 10. Kuoa ama kuwa na mchumba au kuolewa
  - 11. Kukataa adhabu kwa makusudi
  - 12. Utoro

13. Kupata mimba au kuharibu mimba

14. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

### **3.SHERIA NA KANU NI ZA SHULE YA SEKONDARI**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu namba 25 ya mwaka 1978. aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenyne zamana ya elimu nchini.

unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

- (A) Heshma kwa walimu, viomngozi, wazazi wafanyakazi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (B) Mahudhurio mazuri katika kilal shughuli ndani na nje ya shule ni lazima
- (c) Kuwahi katika kila shughuli ya shule na nyingine utakazopewa.
- (D) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipka hiyo wakati wote ukiwa mwanafunzi wa shule hii.
- (E) Kutunza usafi wa mwili na mavazi ya shule .
- (F) Kuvalaa sare ya shule wakati wote utakapotakiwa na kuzingatia ratiba ya shule.